

KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MENEJIMENTI MAALUM KILICHOFANYIKA TAREHE 17/11/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA MJI NEWALA.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA.

1. Ndg. Shamim Mwariko	-Mkurugenzi wa Mji	-Mwenyekiti
2. Ndg. Esther Sanga	-K/Mkuu wa Idara ya Utumishi	-Katibu
3. Ndg. Peter H. Mlaponi	-Mkuu wa kitengo cha Uchaguzi	-Mjumbe
4. Ndg. Salma A. Kisinza	-K/Mkuu wa Kitengo cha Sheria	-Mjumbe
5. Ndg. Humud Mpende	-K/Mkuu wa Idara Elimu Sekondari	-Mjumbe
6. Ndg. Kulwa Mwambilija	-K/Mkuu wa Kitengo cha Ujenzi	-Mjumbe
7. Ndg. Calistus Komba	-Mkuu wa Idara ya Kilimo	-Mjumbe
8. Ndg. Daud Matandiko	-K/Mkuu wa Kitengo cha Tehama	-Mjumbe
9. Ndg. Hyasinty Msanga	-K/Mkuu wa Idara ya Mazingira	-Mjumbe
10. Ndg. Majura Masisa	-K/ Mkuu wa Idara ya Fedha	-Mjumbe
11. Ndg. Winifrida Magubika	-K/Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi	-Mjumbe
12. Ndg. Sophia Makungu	-Mkuu wa Idara ya Mipango	-Mjumbe
13. Ndg. Wilson Fweni	-K/Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili	-Mjumbe

SEKRETARIETI.

1. Ndg. Rajabu S. Madonji	- Katibu wa Kamati
2. Ndg. Grace R. Buttu	- Katibu wa Kamati
3. Ndg. Kamtande Mchemba	- Katibu wa Kamati
4. Ndg. Zubeda H. Likumbo	- Katibu wa Kamati

NTC/TMT. /MUHTASARI NA. 01/2021/2022:- KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 7:11 mchana.

NTC/TMT.3 /MUHTASARI NA. 2/2021/2022:- TAARIFA YA MAPOKEZI FEDHA TZS 470,000,000 ZA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 19 KATIKA SHULE ZA SEKONDARI NA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA KITUO CHA AFYA MNEKACHI KWA KUTUMIA FEDHA ZA PROGRAM YA UVIKO 19.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari aliwasilisha taarifa kwa Wajumbe kwa kuwaeleza kuwa Halmashauri imepokea kiasi cha Fedha Tzs 470 milioni (Fedha za Program ya Uviko 19) kutoka kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya madarasa 19 kwa Shule za Sekondari 11 na nyumba ya mtumishi katika kituo cha Afya Mnekachi katika Halmashauri ya Mji Newala. Aidha, fedha hizo za Ujenzi wa madarasa zimeingizwa kwenye akaunti za Shule husika tarehe 21/10/2021 na fedha za Ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika kituo cha Afya Mnekachi zimeing kama ilivyochanganuliwa hapa chini;

N A	JINA LA SHULE	IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA	KIASI CHA FEDHA KILICHOINGIZ WA
1	DR. ALEX MTAVALA	1	20 MILIONI
2	KIUTA	3	60 MILIONI
3	KUSINI	3	60 MILIONI
4	MAKOTE	1	20 MILIONI
5	MALOCHO	2	40 MILIONI
6	MKUCHIKA	1	20 MILIONI
7	MTANGALANGA	2	40 MILIONI
8	MTUMACHI	2	40 MILIONI
9	NAMBUNGA	1	20 MILIONI
10	NANGWANDA	2	40 MILIONI
11	NEWALA	1	20 MILIONI
12	NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA KITUO CHA AFYA MNEKACHI	3 IN 1	90 MILIONI
	JUMLA	19	470 MILIONI

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuchangia kama ifuatavyo;

Wajumbe walitaka kujua kama fedha hizo ni kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa Shule za Sekondari pekee au Shule za Msingi na wao wamepelekewa.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari alifafanua kuwa fedha hizo zimekuja na mwongozo ambao umeelekeza zitumike kwa Shule za Sekondari tu.

Mwenyekiti alisisitiza kuwa Ujenzi uanze mara moja kama maagizo yalivyotolewa ili kuendana na Muda uliopangwa.

Wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo. Aidha, walishauri kuwe na usimamizi nzuri wa fedha hizo.

NTC/TMT./MUHTASARI NA 3/2021/2022:- KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 8:02 mchana.

"UMETHIBITISHWANA"

Jina.....*George M. Mwaliko*.....

Jina.....*SHAMIRU D. MWALIKO*.....

Sahihi.....*[Signature]*.....

Sahihi.....*[Signature]*.....

Katibu

Mwenyekiti

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI NEWALA**

Tarehe *18*...../...../2021